# UBASHIRI WA JESMA K.C.P.E 2021

010

## - KISWAHILI -

**Machi 2021 - Muda: Saa 1 dakika 40**

**SEHEMU A: KISWAHILI LUGHA**

### SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibu. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala sio katika kijitabu hiki cha maswali.

### JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu:

   **NAMBA YAKO YA MTIHANI**
   **JINA LAKO**
   **JINA LA SHULE YAKO**

6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule. Na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu.
9. Kwa kila swali 1 – 50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C na D. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambayo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

    **Mfano**

    **Katika kijitabu cha maswali:**

    **11.** Sayari ya mwisho kutoka kwa jua ni

    A. mshtara
    B. zebaki
    C. kausi
    D. mirihi

    Jibu sahihi ni C

    1 [A] [B] [C] [D] 11 [A] [B] ▬ [D] 21 [A] [B] [C] [D] 31 [A] [B] [C] [D] 41 [A] [B] [C] [D]

    Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba 11, kisanduku chenye herufi C ndicho kilichochorwa kistari.

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kitabu hiki cha maswali kina kurasa 8 zilizopigwa chapa. Watahiniwa ni lazima wahakikishe kuwa kurasa zote za karatasi ya mtihani zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.**

PREDICTION 2021



Scanned with CamScanner

*Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi* **1** *mpaka* **15.** *Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Jaza kila pengo kwa kuchagua jawabu lifaalo zaidi.*

Suala la uhifadhi wa mazingira __1__ kutiliwa maanani na wanajamii __2__. Ni vyema vijana __3__ kuhusu jambo hili __4__ wakiwa wadogo. Chambilecho wahenga __5__. Wakiachwa wakomae bila kuwajibika, itakuwa __6__ sana kuwatarajia wabadili __7__ zao. __8__ mazingira yetu, sisi __9__ kwa njia nyingi.

**1.** A. unapaswa B. linapaswa C. yanapaswa D. ingepaswa

**2.** A. wengine B. nyingi C. yote D. wote

**3.** A. wausiwe B. wahisishwe C. wakandamizwe D. wabezwe

**4.** A. hadi B. lau C. tangu D. ilhali

**5.** A. papo kwa papo kamba hukata jiwe B. Mtaka mawaridi huvumilia miba
C. mkono mmoja haulei mwana D. Kambare mkunje angali mbichi

**6.** A. ngumu B. vigumu C. gumu D. mgumu

**7.** A. hulka B. hiari C. radhi D. mienendo

**8.** A. Tusivyoyatunza B. Tusipoitunza C. Tusioyatunza D. Tusipoyatunza

**9.** A. ndio tutakaoathiriwa B. ndiyo tutakayoathiriwa
C. ndisi tutakaoathiriwa D. ndisi tutakayoathiriwa

Paulo alikuwa kijana mwenye msimamo __10__. Alikataa katakata kuwa moyo __11__. Marafiki zake __12__ alipoasi kujiunga __13__ katika visa vya utovu wa nidhamu. __14__, hakujali lolote. Alielewa madhara ya shinikizo la rika. Hakutaka kujihusisha na mambo ambayo yangemfanya aishie __15__.

**10.** A. thabiti B. dhabiti C. dhaifu D. kali

**11.** A. bendera inayofuata upepo B. nazi ishindanayo na jiwe
C. mkulima anayewafaa wengi D. daraja linalowavusha watu

**12.** A. walimtwaza B. walimsifu C. walimbeza D. walimtukuza

**13.** A. nasi B. nao C. nanyi D. naye

**14.** A. kwa vile B. hivyo basi C. japo D. hata hivyo

**15.** A. kuenda teki B. kujiuma kidole C. kutia upondo D. kulia ngoa



Scanned with CamScanner

*Kuanzia nambari 16 mpaka 30, chagua jibu lifaalo zaidi*

**16.** Mtu anayechuuza maji huitwaje?

A. Tarishi
B. Mzegazega
C. Mpagazi
D. Mtarijumani

**17.** Badili sentensi hii katika hali ya wingi.

Sonara yule anaugua kifuakikuu.

A. Sonara wale wanaugua vifuavikuu
B. Masonara wale wanaugua vifuavikuu
C. Masonara wale wanaugua kifuakikuu
D. Sonara wale wanaugua kifuakikuu

**18.** Vipi ni viambishi katika neno **chaguliana**?

A. cha-gu-a
B. li-a-na
C. cha-gu-na
D. li-an-a

**19.** Sentensi gani imetumia kiwakilishi cha pekee

A. maduka mengi yamefunguliwa lakini lile limefungwa.
B. wanafunzi wote walihudhuria japo yeye hakufika.
C. tulifika nyumbani humo ila wenyewe hawakuwepo.
D. nilimpa kalamu yangu kwa kuwa yake ilipotea.

**20.** Tambulisha matumizi ya -ji- ya mtendaji

A. uigaji wa mambo ya kigeni umeleta hasara.
B. wanywaji wa pombe wamepewa tahadhari.
C. jibwa hilo linatisha sana.
D. niliketi na kujiuliza maswali.

**21.** Tegua kitendawili: **Baba alinipa mfupa nikautunza ukawa fahali.**

A. muwa
B. ndama
C. mkeka
D. nazi

**22.** Salma ni mke wangu. Dada yangu anaitwa Habiba. Salma na Habiba wataitana

A. dada
B. mpwa
C. mwamu
D. wifi

**23.** Andika ukubwa wa sentensi:

Mkia wa mbuzi ni mfupi.

A. Jikia la jimbuzi ni lifupi.
B. Kikia cha kibuzi ni kifupi
C. Kia la buzi ni fupi.
D. Jikia la jibuzi ni mfupi

**24.** Chagua sentensi ifaayo zaidi.

A. Chai kidogo itanitosha
B. Chai mdogo utanitosha
C. Chai ndogo itanitosha
D. Chai kidogo kitanitosha

**25.** Nomino miwani na miadi huorodheshwa katika ngeli gani?

A. U-I
B. I-I
C. I-ZI
D. U-ZI

**26.** Andika usemi wa taarifa wa sentensi ifuatayo.

"Andikeni kazi hiyo katika vitabu vyenu," mwalimu aliwaambia wanafunzi.

A. Mwalimu aliwaambia wanafunzi kuwa wangeandika kazi hiyo katika vitabu vyao.
B. Mwalimu aliwaambia andike kazi hiyo katika vitabu vyenu.
C. Mwalimu aliwahimiza wawe wakiandika kazi ile katika vitabu vyao.
D. Mwalimu aliwaagiza kuifanya kazi hiyo katika vitabu vyao.



Scanned with CamScanner

**27.** Sheria zinazozingatiwa wakati wa kutunga mashairi huitwa

A. kughani
B. urari
C. mkarara
D. arudhi

**28.** Kipi ni kitenzi kilichoundwa kutokana na nomino?

A. dhoofu-dhaifu
B. cheka-mcheshi
C. bora-ubora
D. unyamavu-nyamaza

**29.** Kauli gani imetumia sitiari?

A. Katule ana urefu wa mlingoti
B. Usiku kucha nilitia nikiota
C. Kusoma ni ibada kwa kila mtoto
D. Mji ulitukaribisha kwa mikono miwili.

**30.** Chagua methali yenye maana tofauti na nyinginezo.

A. Akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki.
B. Damu ni nzito kuliko maji.
C. Mla nawe hafi nawe ila mzaliwa nawe.
D. Isipowasha hunyesha.

Scanned with CamScanner

*Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali* **31-40**

Beti alikuwa msichana mrembo kupindukia. Hata hivyo, methali hapana marefu yasiyokuwa na ncha ilisibu vizuri kwake. Banati huyu alikuwa haambiliki hasemezeki. Fauka ya hayo, alikuwa na tamaa isiyo na kifani.

Alipokuwa katika shule ya msingi, walimu na wavyele walimfunza umuhimu wa kuwa na maadili. Isitoshe, alifunzwa masomo vyema lakini akili yake ilikuwa butu. Akawa haingizi chochote cha maana ila uchafu wa fikira. Nyumbani nako hakuzingatia maonyo. Alikuwa kiguu na njia.

Wakati fulani wa Krismasi, Beti alipomaliza tu shule ya msingi, alikutana na mwanaume mmoja, mliliwa na wasichana wengi, mtajika kwa mali na umbo. Jina lake lilikuwa Bazu. Beti alihadaiwa akahadaika akatorokea kwa huyu Bazu ambaye alikuwa ameshawataliki wake wawili tayari. Akawa mke mlezi. Ikabidi awalee watoto waliobaki na baba yao baada ya mama zao kutanzuka. Awali, Beti aliona raha ingawa alikereka kuitwa mama hata kabla ya kumkopoa mwana wake mwenyewe. Aliwabeza walioukuwepo awali na akajiona kuwa yeye ndiye mchukuzi bora. Akadharau kuwa pakacha likivuja, nafuu huwa ni kwa mchukuzi. Aliwaona wenzake kama maua yaliyonyauka na lake ndilo kwanza linaonana na jua.

Muda si muda, akajikuta ana wana watatu kwa kipindi kifupi. Mumewe naye hakutulia na mambo ya nje. Akaimarisha nyendo zake kiguu na njia, alipochoka, akiingia garini na kuikata mitaa. Beti aende wapi? Alifungika nyumbani ndi! Akamlea mwana huyu na yule, wake na wale wa kambo. Vijisenenesenene vikazidi. Lakini akajaribu kuvumilia akidhani kuwa atazila mbivu, wapi! Alipoligema ilibidi alinywe. Siku zikaja na kupita. Beti akajuta kuwa kutosikiliza wakuu na kumkimbila mtu ambaye hata hakuwa anamwelewa vizuri. Pesa na raha alizokuwa amezikimbilia akawa anazisikia kama hadithi ndotoni. Kwao nako kukawa hakuridhiki. Beti akawa mjamzito tena, kama kawaida akaenda kliniki za wajawazito. Alipopimwa ikabainika kwamba alikuwa na virusi vya ukimwi. Mtoto alipozaliwa akafariki. Mumewe naye, badala ya kumliwaza, akawa wa kumzidishia mzigo kwa kumnyanyasa.

Baada ya miaka mitatu tumbo la Bazu na lile umbo lake likaanza kutoweka. Homa za hapa na pale, vipele,mara kukohoa, kuendesha, yote yakamvamia bila kumpa nafasi. Akamsingizia Beti kuwa ndiye aliyeleta maradhi. Waliokuwa pembe za chaki waliujua ukweli ulipokuwa. **Baadhi ya vidosho wake walishaanza kupukutika kama majani msimu wa mapukutiko**. Pesa zikawaishia Bazu na Beti, hata wakashindwa kutimiza mahitaji muhimu ya kutunza siha zao. Bazu akawa wa kuingia na kutoka hospitali hii na ile huku Beti akijitahidi kuviuguza vidonda ndugu vyake na vya mumewe. Hatimaye mumewe akabwaga chini na ukimwi akafa fo!

Si ndugu si marafiki, hawakumwelewa Beti. Walimwona kama pweza aliyejipalia makaa makubwa ya moto mkali. Ada za shule zikawa ni shida. Huruma ikawaingia watu. Wakasema lisilo budi hutendwa. Wakaubeba mzigo kwa hiari yao. Wakawafanyia watoto harambee ya karo na ada za matibabu. Mwishowe Beti akaungana na mumewe akiwa bado mbichi wa umri. Hata miaka ishirini alikuwa bado hajafikisha. Ikabidi watoto walelewe na wahisani.

Basi jamii hiyo ikaazimia kuwa wao hawatakuwa watumwa wa tabia iletayo UKIMWI. Walitambua kuwa ukongo huu unarudisha nyuma maendeleo na kuipakaza jamii mizigo isiyotarajiwa. Nasi tutahadhari kabla ya hatari.

Scanned with CamScanner

31. Maelezo yapi ni sahihi kulingana na aya ya kwanza?
A. Beti hakupenda kufuata ushauri.
B. Watu wengi walimchukia Beti
C. Beti alikuwa msichana mrembo na mpole.
D. Maumbile ya Beti yalimfanya apotoke.

32. Ni kweli kusema kuwa,
A. wazazi walipuuza wajibu wao.
B. kutoelekezwa kwa Beti kulimfanya apotoke.
C. wazazi walimlea Beti kwa kumdekeza.
D. walimu walitekeleza wajibu wao.

33. Ipi haikuwa sifa ya Bazu kwa mujibu wa kifungu?
A. Aliyeumbika vizuri
B. Mkwasi wa kutajika
C. Mwenye hulka ya kuridhisha
D. Asiyetulia nyumbani

34. Beti alipoolewa na Bazu
A. alikuwa amepata watoto nje ya ndoa
B. alijiona bora kuliko watangulizi wake.
C. aliamua kuwataliki wake wa awali.
D. alikuwa ameshajua tabia halisi ya mumewe.

35. Beti alijua vipi alikuwa akiugua ukimwi?
A. Mtoto wake alipoaga dunia.
B. Alianza kuugua maradhi mbalimbali
C. Alipimwa katika kliniki ya wajawazito.
D. Mumewe alianza kudhoofika kiafya.

36. Dalili za maradhi yaliyotajwa ni pamoja na
A. homa, kukohoa na kuendesha.
B. mafua, upele na kubambuka ngozi.
C. kukonda, kuendesha na kifua.
D. kudhoofika kiafya, kukonda na kusambaza.

37. '**Baadhi ya vidosho wake walishaanza kupukutika kama majani msimu wa mapukutiko**.' Maana ya kifungu hiki ni kuwa,
A. baadhi ya marafiki wa Beti walianza kufariki.
B. wapenzi wa Bazu walianza kuaga dunia.
C. waliokuwa marafiki wa Bazu na Beti walianza kujitenga
D. Wasichana warembo wa kijiji walianza kuugua mmoja mmoja.

38. Jamii ya akina Beti inajaliana maslahi kwa kuwa,
A. inahamasisha watoto kuhusu maradhi ya UKIMWI
B. inatoa michango kwa wanaougua UKIMWI.
C. inawaona kama pweza wanaojiingiza matatani.
D. inawahudumia mayatima kwa njia ifaayo.

39. Kulingana na kifungu, ugonjwa wa UKIMWI unasambazwa zaidi na
A. wanaume matajiri, wasichana walio chini ya umri.
B. watu wasio na elimu, wanaume wenye wake wengi.
C. kutowajibika kwa vijana, watu wasio waaminifu katika ndoa.
D. watu wasiotulia nyumbani, wasichana warembo.

40. Kichwa kinachofaa kwa habari hii nii,
A. Mpanda ngazi hushuka.
B. Baada ya dhiki faraja.
C. Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu.
D. Penye urembo ndipo penye ulimbo.

Scanned with CamScanner

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali kuanzia nambari* **41** *mpaka* **50**

Usidharau wembamba wa reli garimoshi hupita, wazee wa jadi wenye busara walilonga. Vijana humu nchini wana uwezo si haba wa kuchangia katika maendeleo pindi tu wapate fursa mwafaka. Katika maendeleo pindi tu wapate fursa mwafaka. Katika jamii yoyote ile vijana ndio huwa na mikikimikiki, sifa ambayo huwawezesha kukabiliana na changamoto nyingi ikilinganishwa na kundi jingine lolote.

Mojawapo ya majukumu ya vijana katika taifa lolote ni kushiriki katika zaraa. **Kilimo ni uti wa mgongo** wa mataifa mengi yanayoendelea hasa katika bara la Afrika. Kupitia kupewa mafunzo mwafaka, vijana wanaweza kutumia nguvu zao kuendeleza kilimo. Shughuli hii itaepushia jamii ya baa la jaa. Isitoshe, mazao ya ziada yanaweza kuuzwa na jamii kujipatia mapato yanayoweza kukimu mahitaji tumbitumbi.

Viongozi wakongwe hawana budi kuwashirikisha vijana katika shughuli za uongozi. **Kinolewacho hupata**. Vijana hawa watapata tajriba muhimu itakayowaandaa kuwa viongozi wema wakati viongozi watakapoondoka mamlakani.

Mara nyingi vijana wamesikika wakikashifu viongozi wazee. Madai yao huwa kwamba viongozi wazee hawawajali kwa hivyo, wang'atuke madarakani wawapishe. Vijana wakumbuke kuwa wazee hawa walikuwa vijana pia na labda wao nao waliwafokea waliowatangulia wakiwataka waondoke. Uongozi hupokezanwa hatua kwa hatua. Busara na hekima mara nyingi hutegemea tajriba ya mja maishani. Nao vijana hawana budi kuwaheshimu viongozi wazee kwani zamu yao itafika.

Vilevile, ni wajibu wa vijana kujitia moyo na kufanya kazi kwa bidii ili kujenga nchi. Wao wanapaswa kujiepusha na mazoea mabaya ya kutofanya kazi na kupenda starehe na vitu vya bure. Aidha, vijana wanatakiwa kuepukana na maovu ya kijamii kama uasherati na matumizi ya mihadarati. Ikiwa vijana watafuata dira maadili mema, mustakabali wao utaingia mwanga wa matumaini.

Vijana ni lazima waongoze katika harakati za biashara na katika nyanja mbalimbali za uvumbuzi, hasa teknolojia kupitia haya, watakuwa wamefaulu kuwatengenezea wananchi nafasi chungu nzima za kuimaraisha hali ya uchumi wa nchi.

Utamaduni hafifu ni mojawapo ya mambo yanayokwaza maendeleo ya taifa, hasa ule unaowanyima wasichana fursa ya kuelimishwa. Wanaofuata utamaduni huu hawatambui kuwa ni hatia, si hatua. Vijana wana wajibu wa kuhakikisha kuwa masuala ya kitamaduni yanayokwaza maendeleo yametupiliwa mbali. Baadhi ya tamaduni hizi ni tohara za wasichana na kuozwa kwa nguvu. Elimu kwa mtoto wa kike ni muhimu kwani ukimwelimisha umeelimisha jamii nzima.

Mwishowe, wahenga hawakutuvisha kilemba cha ukoka waliponadi kuwa samaki mmoja akioza huoza wote. Miongoni mwa vijana walioadilika na kuwajibika kunao walio jeuri mithili ya mabeberu na wenye utovu wa nidhamu. Wengi wao wamejihusisha na uhalifu. Wengine hutumiwa na viongozi waovu kueneza ghasia. Vijana waadilifu wana wajibu wa kuwaelekeza waliopotoka. Wawe cheche ya kuleta moto wa **mabadiliko chanya**. Hivyo, watakuwa vyombo vya kuleta maendeleo.

Scanned with CamScanner

41. Mwandishi ameanza kwa kusema kuwa
A. vijana hawafai kudharau wazee wa jadi.
B. uwezo wa vijana sio wa kupuuzwa.
C. uongozi unafaa kuachiwa vijana pekee.
D. reli ikiwa nyembamba ni nzuri zaidi.

42. Kauli **kilimo ni uti wa mgongo** imetumia tamathali gani ya usemi?
A. tashbihi
B. nahau
C. chuku
D. sitiari

43. Umuhimu wa kilimo kulingana na makala haya ni
A. kujitosheleza kichakula, kujipatia fedha.
B. kuwapa vijana mafunzo, kuondoa njaa.
C. kupata mauzo, kupunguza mahitaji
D. kuwashirikisha vijana, kununua chakula.

44. Vijana hawafai kuwakashifu wazee kwa kuwa
A. nafasi yao ya uongozi haijafika.
B. wazee ndio wanafaa kuongoza jamii
C. wazee hawawezi kung'atuka uongozini.
D. wao pia watakuja kuzeeka

45. Maoni ya mwandishi ni kuwa
A. vijana wasiachiwe mamlaka kwa kuwa hawawajibiki.
B. vijana wote huwa na kipawa cha uongozi.
C. aghalabu maarifa huongezeka kadri mtu anavyoishi.
D. mtu akizeeka sana hupungukiwa na ujuzi.

46. Methali **kinolewacho hupata** ina maana kuwa,
A. vijana wakishirikishwa mapema wataimarisha uwezo wao wa kuongea.
B. wazee wakiendelea kutawala watajiongezea maarifa zaidi.
C. viongozi waliopo wakiondoka uongozi wa vijana utaimarika.
D. vijana wakihusishwa ipasavyo, watambue nafasi ya wazee katika jamii.

47. Katika aya ya **tano**, mwandishi anapinga,
A. hali ya vijana kupewa vitu bure.
B. mgogoro uliopo baina ya vijana na wazee.
C. vijana wanaofuata dira ya maadili mema.
D. mazoea ya vijana wanaolaza damu.

48. Msichana akipewa nafasi ya kuelimika;
A. atachukua nafasi za uongozi badala ya mvulana.
B. atachangia katika kuimarisha jamii pana zaidi.
C. utamaduni wa Mwafrika utadidimizwa.
D. atafanya vyema kuliko mtoto wa kiume.

49. Vijana kwa jumla wanahimizwa
A. wangoje wazee wang'atuke uongozoni kwanza.
B. wazingatie mchango wao katika maendeleo.
C. watumie teknolojia badala ya kuingilia kilimo.
D. Washirikiane na wale walio na hulka mbovu.

50. **Mabadiliko chanya** ni;
A. Mabadiliko mabaya
B. Mabadiliko ya kiuchumi
C. Mabadiliko yanayofaa
D. Mabadiliko ya tabia

Scanned with CamScanner